



## TAARIFA KWA UMMA

### TATHMINI YA ATHARI ZA ONGEZEKO LA BEI YA MAFUTA KATIKA USAFIRI WA ABIRIA MAJINI

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) linuarifu umma kuwa linafanya tathmini ya athari za mabadiliko ya bei elekezi za mafuta zilizoanza kutumika tarehe 1 Aprili 2026. Lengo la tathmini hii ni kubaini iwapo kuna haja ya kurekebisha nauli za abiria katika njia mbalimbali za usafiri wa majini.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, TASAC itawashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni katika mchakato unaoendelea. Vikao vya wadau vitafanyika tarehe 16 Aprili, 2026 kama ifuatavyo:

- (i) Ukerewe - Ukumbi wa Millenium Plaza
- (ii) Kigoma - Ukumbi wa Kigoma Social Hall
- (iii) Kagera – Ukumbi wa ELCT bukoba

Vikao vyote vitaanza saa 4:00 asubuhi.

Aidha, wadau wanakaribishwa kuwasilisha maoni yao kwa maandishi kuhusu athari za mabadiliko ya bei ya mafuta na mapendekezo ya hatua stahiki za kuchukua. Maoni yawasilishwe kupitia:

- (i) Barua pepe: [tariff@tasac.go.tz](mailto:tariff@tasac.go.tz)
- (ii) Anwani ya posta: Mkurugenzi Mkuu, TASAC, S.L.P. 989, Dar es Salaam

Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 26 Aprili 2026.

**Imetolewa na:**  
**Mkurugenzi Mkuu,**  
**TASAC**